**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI**

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na. HW/MUF/S.40/3 VOL.II/28** **04/07/2025**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi anapenda kuwatangazia wakazi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi wenye nia ya kufanya kazi za Ajira ya Muda (Vibarua) kwa nafasi ya wakusanya mapato kwa Vijiji vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

### 1.0 NAFASI 94

### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe ni Mtanzania na mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
2. Mwombaji awe amehitimu Kidato cha IV na kupata cheti cha matokeo (School Certificate).
3. Mwombaji awe amepitia mafunzo ya taaluma yeyote katika ngazi ya kuanzia Astashahada na kuendelea, wenye fani ya kodi, biashara, Uhasibu, Mipango, Sheria, Maendeleo ya Jamii nk. watapewa kipaumbele.
4. Awe na uwezo wa kutumia kompyuta/Simu janja.
5. Awe na wadhamini **watatu (3)** ambao ni lazima wawe watumishi wa Serikali au wanaotambulika vema katika jamii ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.
6. Watumishi wanaojitolea ndani ya Halmashauri ya Mufindi na waliopitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa watapewa kipaumbele.

### 1.2 KAZI ZA KUFANYA

1. Kukusanya ushuru unaotokana na mazao ya misitu, mazao ya kawaida, madini (mchanga, kokoto, mawe) katika Kijiji ambacho atapangiwa ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.
2. Kuwasilisha benki fedha inayotokana na makusanyo hayo kila siku.
3. Kufanya usuluhishi wa kibenki katika POS.

OfisiyaMkurugenziMtendaji S.L.P 223, Mafinga, Simu: +255262772614, Nukushi: +255262772070.

BaruaPepe :ded@mufindidc.go.tz, Tovuti: http://www.mufindidc.go.tz

CamScanner

### 1.3 MALIPO

Malipo yatakuwa Tshs. 10,000/= kwa siku na malipo yatafanyika mwisho wa mwezi.

### 2.0 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

i. Maombi yapitishwe kwa Watendaji wa Vijiji kuthibitisha uhalali wa mhusika.
ii. Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vya Elimu na Taaluma kama inavyoelekezwa hapo juu. Kitambulisho cha Taifa (NIDA), picha mbili (Passport size za sasa).
iii. Awe na wadhamini ambao ni lazima wawe watumishi wa Serikali au watu wanaotambulika katika Jamii ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi wenye mali isiyohamishika inayoweza kutumika kama dhamana ikitokea mwombaji amepata kazi na akakiuka masharti ya ajira yake.
iv. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **14/07/2025** Saa 09:30 alasiri.
v. Muombaji asiyefuata maelekezo atakuwa amejitoa katika nafasi ya kufikiriwa kuitwa kwenye usaili.

Maombi yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili/Kiingereza fasaha na kuwasilishwa kupitia **Masijala ya wazi** Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi au yatumwe kupitia anuani ifuatayo;-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi,
S.L.P 223,
**MAFINGA.**

Imetolewa na:-

MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI S.L.P. 223, MAFINGA

Daniel S. Mapilya
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**MUFINDI**

**Nakala:** Mbao za Matangazo
: Tovuti ya Halmashauri www.mufindidc.go.tz



CamScanner